# MATTERS OF THE BLOOD

## (MAMBO YAHUSUYO DAMU)

LAANA NA BARAKA ZA FAMILIA.

**Pastor, Tony Osborn**

**© March 2024 Pastor Tony Osborn**

Kitabu hiki kimeandikwa na **PASTOR TONY OSBORN**. Haki zote zimehifadhiwa, huruhusiwi kunakili, kurudufu au kutumia sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi.

Kufanya hivyo itakuwa ni Ukiukwaji wa taratibu na hii inaweza kukupelekea kushtakiwa kutoka kwa waandaaji wa kazi hii.

**Pastor, Tony Osborn**

**Dar es salaam, TANZANIA (Afrika Mashariki)**

**Simu: 0762153539/0659085731**

**Instagram / Tiktok: Pastor Tony Osborn**

# YALIYOMO:

**SHUKRANI.......................................................................................vi**

**SEHEMU A: MAMBO YAHUSUYO DAMU YA FAMILIA ................. 1**

**SURA YA 1: MAANA YA DAMU YA FAMILIA..................................2**

1.1 KWANINI DAMU? ......................................................................5

1.2 NAMNA AMBAVYO MUUNGANIKO WA DAMU UNAWEZA KUATHIRI MAISHA YA MTU........................................................20

**SURA YA 2: DAMU YA YESU..........................................................23**

2.1. KAZI YA DAMU YA YESU KATIKA KUTUKOMBOA NA MUUNGANIKO WA DAMU ZA FAMILIA....................................24

Kazi ya 1: Kutununua kwa Damu yake ................................................24

Kazi ya 2: Kutuhamisha Kutoka falme za giza......................................26

Kazi ya 3: Kutuingiza katika Ufalme wake............................................27

Kazi ya 4: Kutufanya watu wapya na wenye haki mbele zake ................28

**SEHEMU B: UFAHAMU JUU YA SOMO LA LAANA.......................30**

**SURA YA 3: LAANA NI NINI? ......................................................... 31**

3.1. CHANZO & MWANZILISHI WA LAANA ...............................34

3.2. NAMNA AMBAVYO LAANA INAFANYA KAZI ....................48

**SURA YA 4: DALILI ZA MTU ANAYETEMBEA CHINI YA LAANA..........................................................................................56**

4.1. MTU ALIYELAANIWA YUPOJE? ...........................................68

4.2. JE, NI KWELI MTU ALIYEOKOKA ANAWEZA KUISHI CHINI YA LAANA? ....79
4.3. MADHARA NA ATHARI YA KUISHI CHINI YA LAANA ....80

**SURA YA 5: AINA NA MAKUNDI YA LAANA .... 86**
5.1. LAANA YA MUNGU ....86
SABABU ZINAZOMFANYA MTU ALAANIWE NA MUNGU. ....91
5.2. LAANA YA KISHETANI NA KICHAWI ....108
SABABU ZA LAANA YA KISHETANI / KICHAWI ....109
5.3. LAANA YA WANADAMU WENYEWE ....113
SABABU ZINAZOMFANYA MTU AJILAANI YEYE MWENYEWE ....114

**SEHEMU C: .... 129**
**LAANA & VIFUNGO VYA FAMILIA .... 129**
**SURA YA 6: MAANA YA LAANA & VIFUNGO VYA FAMILIA . 130**
Laana na vifungo vya familia ni nini? ....130
Vifungo vya familia ni nini? ....134
6.1. CHANZO CHA LAANA NA VIFUNGO VYA FAMILIA ....135

**SURA YA 7: DALILI YA LAANA & VIFUNGO VYA FAMILIA .. 145**
7.1. ATHARI & MADHARA YA KUISHI CHINI YA LAANA NA VIFUNGO VYA FAMILIA ....156



**SURA YA 8: MUONGOZO WA MAOMBI YA KUKUTOA KATIKA LAANA NA VIFUNGO VYA FAMILIA .... 164**

MAOMBI YA KUMPOKEA YESU KUWA BWANA NA MWOKOZI WA MAISHA YAKO........................................................168

8.1. MAOMBI YA TOBA ....................................................................170

8.2. MAOMBI YA KUVUNJA KILA KIFUNGO NA LAANA YA FAMILIA INAYOKUFUATILIA ......................................................177

8.3. MAOMBI YA KUFUTA NA KUTENGUA KILA MANENO YA LAANA YALIYOTAMKWA JUU YAKO ........................................180

8.4. MAOMBI YA KUJITENGANISHA NA UKOO WENU .........184

8.5. MAOMBI YA KUFUNGA MILANGO INAYORUHUSU LAANA KUINGIA KWAKO ...........................................................186

8.6. MAOMBI YA SHUKRANI ..........................................................189

**SURA YA 9: KUACHILIA BARAKA ZA MUNGU KWA FAMILIA ZETU ............................................................................................. 194**

**HITIMISHO............................................................................... 200**

# SHUKRANI:

Ninamshukuru Mungu sana kwa uaminifu wake na kwa kunijalia ROHO MTAKATIFU ambaye kwa mafunuo yasiyo ya kawaida amenipa NEEMA ya kuandika kitabu hiki kilichobeba mafunuo na siri nyingi sana juu ya somo zima ushirika uliokuwepo kati ya mtu na muunganiko wa damu ya familia na somo la laana na hasa laana za familia ambazo zimekuwa zikiwatesa wengi.

Siri zilizoandikwa humu kwa uwezo wa Roho wa Mungu zitakusaidia na kukuongoza hatua kwa hatua kutoka katika vifungo na laana za familia na kuvuta Baraka ya Mungu kuja juu ya maisha yako.

Neno la Mungu linasema katika kitabu cha;

**Marko 2:21-22**

**"Watu hawakati kiraka cha nguo mpya na kukishonea katika nguo kuukuu. Kama wakifanya hivyo, hicho kiraka kipya kitararuka kutoka hilo vazi kuukuu, nalo litaharibika zaidi. Wala watu hawatii divai mpya katika viriba vikuukuu. Kama wakifanya hivyo, divai itavipasua hivyo viriba, nayo divai pamoja na hivyo viriba vitaharibika. Divai mpya hutiwa katika viriba vipya!"**

Hii inaonyesha ya kuwa kuna maeneo mengi katika maisha yetu hatuwezi kuvuka isipokuwa kwa kuondoa kiriba kikuukuu (laana na vifungo) ili tuweze kupata kibali cha kupokea Baraka na mafanikio katika maisha yetu.

Kitabu hiki ni mkusanyiko wa Mafunuo na Maombi yote yahusuyo somo la laana na Baraka za familia na ni kwa namna gani utajitoa katika laana na kuivuta Baraka ya Mungu kwako na familia yako.

Shukrani zangu za pekee ziwafikie watoto wangu wa kiroho wote, ndani na nje ya nchi ya Tanzania, kwa kunipenda, kuniombea na zaidi ya yote kunipokea na kuniamini, Kumuamini Mungu aliyeniita na huduma iliyopo ndani yangu.

Ninawashukuru sana kwa kuwa nyie mmenipa nafasi katika mioyo yenu na kuamini kile kitu na huduma Mungu ameweka ndani yangu.

Ninawapenda, ninawaombea na Mungu wa mbinguni awabariki sana.

Kiupekee kabisa ninamshukuru mke wangu mpenzi Mrs Neema Tony Kapola ambaye amekuwa akikesha pamoja nami, akisukuma na kusimamia kwa ufasaha ukamilifu wa kitabu hiki. Ninakupenda na Asante kwa kusimama na mimi katika wito na kazi hii ambayo Mungu amenipa.

Mungu aendelee kukuonekania wewe na familia yako ndani ya mwaka huu.

*Amen……………………*

**-Pastor Tony Osborn**

# SEHEMU A: MAMBO YAHUSUYO DAMU YA FAMILIA

# SURA YA 1: MAANA YA DAMU YA FAMILIA

*Nini maana ya Damu ya familia? Hii damu ya familia inafanyaje kazi ndani ya maisha ya mtu?*

Tunapoongelea damu ya familia huwa tunaongelea muunganiko wa kibaiolojia na wa kiroho kati ya watu ambao wamezaliwa katika familia moja yaani baba, mama na watoto na wengineo.

Damu ya kifamilia tunaweza kuiongelea katika mitazamo mikuu miwili ambayo ni;

- **Mtazamo wa kibaiolojia.**

Katika mtazamo wa kibaiolojia damu ya familia huusisha ushirikiano wa vinasaba kati ya wazazi na watoto watakaozaliwa katika hiyo familia. Kitaalamu zaidi huitwa DNA.

Katika baiolojia kwa asilimia 99.99% mtoto hurithi vinasaba Kutoka kwa wazazi wake na hii humaanisha kuwa; kuna vitu Kutoka kwa baba na mama vinaunganika na kisha kumuunda huyo mtoto.

Hivyo kama ikitokea damu ya baba au mama ilikuwa na shida ya magonjwa ambayo yanaweza kurithishwa kama vile pumu, sickle cell, kansa, kifafa, magonjwa ya upofu na mengineyo mtoto atakayezaliwa ana asilimia kubwa na yeye kuyapata magonjwa ya aina hii kwa sababu ya ule ushirika wa damu.

Ndio maana sio ajabu kukuta babu alikuwa na pumu, baba akawa na pumu, watoto nao wakawa na pumu na wajukuu na kizazi kijacho kikawa kinasumbuliwa na shida hiyo hiyo au unakuta familia nzima wanasumbuliwa na kansa na kila anayekufa anakufa kwa huu ugonjwa.

Kibaiolojia hili ni jambo linalowezekana kabisa, lakini wataalamu wanasema pia kuwa ukiachana na magonjwa mtu anaweza pia kurithi tabia au uwezo wa akili Kutoka kwa wazazi.

*Mfano,* baba anaweza akawa anapenda somo la hesabu na akawa na uwezo nalo sana kuliko masomo mengine na ukashangaa baadhi ya watoto atakaowazaa au watoto wote wakawa wanapenda somo la hesabu na kuliweza zaidi kuliko masomo mengine. Hii haitokei kwa bahati mbaya ni swala la kurithishana vinasaba.

Mfano mwingine unaweza kukuta familia ambazo wao kwao kila mtu ni daktari, mwanasheria au mwalimu, yaani kila anayezaliwa katika hiyo familia anajikuta anapenda kufanya hizo kazi na hata ukitafuta mtu mwenye ujuzi mwingine au utaalamu mwingine unaweza usimpate au ukawapata wachache sana.

Haya yote yanawezekana tu kama kutakuwa kuna muunganiko wa damu ambao unasababisha vinasaba kusafiri Kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine.

- **Mtazamo wa Kiroho.**

Swali la msingi la kujiuliza ni kuwa; kama kibaiolojia inawezekana kwa mambo makubwa kama haya kutokeo vipi kuhusu mtazamo wa damu ya familia katika ulimwengu wa roho?

Tukija upande wa rohoni, tunaangalia zaidi mambo ya rohoni yanavyoshirikiana na damu katika kuathiri maisha ya mtu.

Kwanza kabisa tukumbuke ya kuwa sisi ni watu wa rohoni, hivyo kama sisi tu watu wa rohoni maana yake ni kuwa tunavyo na sisi vinasaba vya

rohoni, tabia za rohoni ambazo zinaweza kusafiri kizazi kimoja hadi kingine.

Hapa ndipo tunapokutana na Laana za familia, magonjwa ya familia, shida, mikosi na mabalaa katika familia ambazo chanzo chake kikubwa ni rohoni.

Kwahiyo, tofauti kubwa katika mitazamo hii miwili ni kuwa;

-Mtazamo wa kibaiolojia unasababishwa na sababu za kibaiolojia ambazo kwa namna nyingine tunaweza kusema hazizuiliki na

-Mtazamo wa kiroho unasababishwa na sababu za kiroho ambazo zinaweza zikazuilika au kuondolewa katika maisha ya mtu.

Hapa ndipo tunapokutana na changamoto kama hizi zifuatazo.

- **Kwenu hakuna changamoto ya utasa na wala hakuna shida ya uzazi ila unakuta watu wanahangaika kupata watoto au hawapati kabisa.**
- **Wengine familia zao kila wakibeba mimba watoto wanakufa na wakienda hospitali wanaambiwa wako sawa na hata Rhezuz factor (RH) zao ziko sawa kabisa.**

*Nini kinasababisha hili?*

Hapa ndipo somo la Damu za familia katika mtazamo wa kiroho linapoanzia.

## 1.1 KWANINI DAMU?

Tunasoma katika kitabu cha;

**Waebrania 12:24**

**“na Yesu mjumbe wa agano jipya, na damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habili.”**

Kwanza kabisa neno la Mungu linasema; **DAMU HUWA INANENA.** Ukisoma vizuri hapo anaonyesha ya kuwa damu ya Yesu huwa inanena mema kuliko ile ya habili, maana yake ni kuwa kuna damu zingine ambazo huwa hazineni mema au